

斯瓦希里语 口语教程

MAZUNGUMZO
YA
KISWAHILI

冯玉培 编著



外语教学与研究出版社

11823
1

MAZUNGUMZO YA KISWAHILI

斯 瓦 希 里 语 口 语 教 程

冯玉培 编著

外语教学与研究出版社

WORLD BOOK PUBLISHING CO., LTD.

(京)新登字 155 号

图书在版编目(CIP)数据

斯瓦希里语口语教程/冯玉培编著. —北京:外语教学与研究出版社, 2003

ISBN 7-5600-3393-8

I. 斯… II. 冯… III. 斯瓦希里语—口语—教材 IV. H823.94

中国版本图书馆 CIP 数据核字(2003)第 046946 号

斯瓦希里语口语教程

编著: 冯玉培

* * *

责任编辑: 曹 勤

出版发行: 外语教学与研究出版社

社 址: 北京市西三环北路 19 号 (100089)

网 址: <http://www.fltrp.com>

印 刷: 北京外国语大学印刷厂

开 本: 850×1168 1/32

印 张: 11.25

版 次: 2003 年 6 月第 1 版 2003 年 6 月第 1 次印刷

书 号: ISBN 7-5600-3393-8/G·1672

定 价: 14.90 元

* * *

如有印刷、装订质量问题出版社负责调换

制售盗版必究 举报查实奖励 (010)68917826

版权保护办公室举报电话: (010)68917519

前 言

这本《斯瓦希里语口语教程》，是为中国学生学习斯瓦希里语而编写的，旨在提高学生的口语表达能力和交际能力。本书供大学二年级使用，也可供有一定斯瓦希里语基础的人自学。

本书共包括 26 课，主要以日常生活内容为主。每课分 4 个部分：1、情景对话（2-5 组）；2、短文（1-2 篇）；3、词汇及相关词语；4、综合练习。情景对话都是在日常语言交际中常用的表达方式，地道、规范、生动活泼；短文内容丰富、题材广泛，并配有问答题及讨论题；综合练习中的语法部分，采取与《斯瓦希里语》精读教材第二册同步，由易到难、循序渐进的原则，有助于学生复习、巩固精读课所学的语法知识。

本书重点突出了实用性，通过对话、叙述、问答、讨论等多种训练，提高学生的口语表达能力。学完本书，可以满足日常交际的基本需要，并为进一步提高学生的口语水平打下基础。

在本书的编写过程中，得到了坦桑尼亚在华专家埃玛努尔·莫莱尔先生和桑给巴尔萨罗姆·赛义夫先生的帮助，北京外国语大学曹勤老师审阅了全书，并提出了许多宝贵意见，在此一并表示诚挚的谢意。

限于编者水平，书中之不足在所难免，恳请读者批评指正。

编者

2003 年 4 月

YALIYOMO 目录

1. Maamkizi na Adabu 问候与礼节	1
2. Kutambulisha na Kujitambulisha 介绍与自我介绍	17
3. Mazungumzo Juu ya Wakati, Tarehe na Majira 谈论时间、日期 和季节	30
4. Kuonana na Daktari 看病	44
5. Posta 在邮局	59
6. Maelekezo ya Njia na Mahali 问路	72
7. Kumkaribisha Mgeni 招待客人	84
8. Kununua Tikititi 购票	96
9. Hotelini 在旅店	106
10. Hali ya Hewa 天气	118
11. Usalama wa Raia 治安	131
12. Usafiri 交通	147
13. Uhamiaji 海关/移民局	161
14. Kununua Vitu 购物	174
15. Katika Benki 在银行	192
16. Kupiga Simu 打电话	206
17. Sikukuu 节日	217
18. Matembezi na Utalii 参观旅游	232
19. Kutafuta Kazi 求职	248
20. Upishi 烹饪	260
21. Hifadhi ya Mazingira 环保	272

22.	Mazungumzo Juu ya Kiswahili 谈论斯瓦希里语	284
23.	Chuo/Shule 学校	298
24.	Utamaduni na Burudani 文化娱乐	314
25.	Uchumba na Ndoa 婚恋	325
26.	Michezo 体育	338

Somo la Kwanza

Maamkizi na Adabu

- Mama Juma: Hodi! Hodi tena! Wenyewe wapo?
- Mama Ali: Karibu Mama Juma.
- Mama Juma: Asante.
- Mama Ali: Je, umeshindaje?
- Mama Juma: Salama tu. Je, bwana na watoto hawajambo?
- Mama Ali: Hawajambo. Kaa kitako, tafadhali. Mbona umesimama wima tu?
- Mama Juma: A-a, nimeacha chungu jikoni. Nimekuja kukujulieni hali tu. Haya, kwa heri.
- Mama Ali: Kwa heri ya kuonana, nisalimie watoto.
- Mama Juma: Sawa, nitawasalimia.
- * * *
- Kidawa: Hodi hapa!
- Asha: Karibu shoga yangu.
- Kidawa: Habari za siku nyingi?
- Asha: Njema, zako tu?
- Kidawa: Ah, hivyo hivyo, hauchi unakucha.
- Asha: Huonekani, kama uko Maka?
- Kidawa: Nipo, siku hizi shughuli zimezidi.
- Asha: Karibu chai.

Kidawa: Asante. Wewe endelea tu, mimi naondoka.

Asha: Kwa nini hukai tukazungumza?

Kidawa: La, sikai. Tutaonana siku nyingine. Nimemwacha mama peke yake.

Asha: Haya, nisalimie mama yako.

Kidawa: Sawa. Kwa heri.

Asha: Kwa heri.

* * *

Mama: Asha, mbona umekawia kuja. Kuna nini huko chumbani?

Asha: Samahani mama. Mimi na mdogo wangu tunasukana nywele.

Mama: Mbona uso wako hauna tabasamu, kwani umeamkaje?

Asha: Nimeamka vema, mama.

Mama: Au kichwa bado kinakuuma.

Asha: La mama, kimepoa.

Mama: Je! Una tatizo lolote lile?

Asha: Sina mama.

Mama: Basi nenda dukani ukaninunulie sukari.

Asha: Sawa. Nakwenda sasa hivi.

* * *

Mtoto: Shikamoo babu!

Mzee: Marahaba, mjukuu wangu.

Mtoto: Je, babu, u hali gani?

Mzee: Hali yangu ndivyo hivyo hivyo, leo mzima, kesho mgonjwa. Unajua, uzee ni nyumba ya maradhi. Lakini nashukuru, naweza kujikongoja kwenda huku na huku.

Mtoto: Mungu atakuafu, atakupa uzima.
 Mzee: Asante.
 Mtoto: Je, umesafiri salama?
 Mzee: Safari yangu ilikuwa salama salimini.
 Mtoto: Karibu nyumbani. Hebu nikutengenezee kikombe cha chai.
 Mzee: Asante. Lakini wazee wako wapi?
 Mtoto: Wamekwenda kukata kuni.
 (baada ya kunywa chai)
 Mzee: Nashukuru kwa kunikirimu chai. Sasa naondoka.
 Mtoto: Haya, kwa heri, karibu tena.
 Mzee: Asante.

* * *

Hassan: Hodi! Hodi! Wenye nyumba wapo?
 Abdalla: Karibu! Ninakuja!
 Hassan: Habari za kushinda?
 Abdalla: Salama tu. Samahani, nilikuwa huko uani. Mtu akipiga hodi ni shida kusikia. Hujambo?
 Hassan: Sijambo. Je, Hamisi yupo? Tumepanga kwenda mpirani.
 Abdalla: Ameniambia. Ngoja nimwite.
 Hamisi: (Akitokea kutoka chumbani) Je, ndugu Hassan, habari za kutwa, umeshindaje?
 Hassan: Salama tu. Je, habari za tangu jana?
 Hamisi: Nzuri tu. Mimi niko tayari. Twende zetu.
 Hassan: Haya, twende. Kwa heri kaka Abdalla.
 Abdalla: Kwa heri ya kuonana.

Maneno ya Heshima

Siku moja Juma na mwalimu wake walikwenda mjini. Toka nyumbani kwa mwalimu mpaka mjini ni mwendo wa saa moja. Juma alifurahi kufuatana na mwalimu wake. Alijua kuwa atajifunza mengi kwa kufuatana na mwalimu. Baba yake aliwahi kumwambia kuwa mtu anaweza kujifunza mengi mahali popote.

Walipoanza safari yao, Juma alimsaidia mwalimu kuchukua mfuko wake. Mwalimu alifurahi sana na kusema, “Nakupenda sana, Juma, utakuwa mtoto mzuri na mwenye adabu na heshima.”

Juma: Asante, mwalimu. Mimi nataka niwe mtoto mwenye tabia nzuri.

Mwalimu: Fanya bidii. Waswahili husema, “penye nia pana njia”.

Juma: Mwalimu, nina maswali machache. Naomba niyaulize wakati tunapotembea ili tufike mjini bila kuchoka.

Mwalimu: Yaulize tu, Juma.

Juma: Watu hutumia maneno haya: “tafadhali”, “samahani”, “pole”, “niwie radhi”, “hongera” na “asante”, lakini sijui ni wakati gani tuyatumie maneno haya.

Mwalimu: Hili ni swali zuri sana Juma, na utakapoweza kuyatumia vizuri maneno haya utaishi vizuri na watu. Pia watu watakupenda. Watu wanapenda watoto wenye heshima na adabu. Sasa nikueleze matumizi ya neno moja moja. Tuanze na neno “tafadhali”. “Tafadhali” hutumiwa wakati unapomtaka mtu akufanyie jambo fulani. Kwa mfano, kama una kiu na unataka maji, unasema, “Tafadhali naomba maji ya kunywa.” Hii ni heshima na mtu akisikia maneno hayo

atafurahi.

Juma: Ni hivyo tu.

Mwalimu: Hapana. Kuna matumizi mengine. Kama mtu amesimama njiani na unataka kupita, unamwomba akupishe kwa kusema, “Tafadhali naomba nipite.” Haifai kumsukuma tu au kumpiga kikumbo. Hivyo “tafadhali” hutumiwa pia katika kuomba njia. Unapomwomba mtu akufanyie jambo fulani au akuhudumie, unatumia neno “tafadhali”, na hapo unaonekana kuwa una heshima.

Juma: Asante mwalimu, nimeelewa wapi nitumie “tafadhali.” Sasa, tafadhali nieleze ni wakati gani tunatumia “samahani.”

Mwalimu: Vizuri. “Samahani” hutumiwa kama umemsumbua mtu au umemwumiza au umemwudhi mtu. Kama umemwomba mtu akufanyie kazi, hii ina maana kuwa umemsumbua. Hivyo unamwambia “samahani” kwa kumsumbua. Kama umemkanyaga mtu bila kukusudia, au umemwumiza mtu bila makusudi unampa “pole” na “samahani.” Hakikisha kuwa hutarudia tena kutenda jambo hilo. “Pole” huonyesha heshima, adabu na upendo. Kama mtu amekuwa mgonjwa na unaambiwa habari zake unampa “pole.” “Pole” pia hutumiwa kama umemwumiza mtu. “Pole” inaonyesha kuwa unawapenda na kuwajali wenzako. Pia baba anapotoka shambani na kurudi nyumbani inafaa kumpa “pole” kwa kazi ngumu aliyofanya.

Juma: Je, na mimi nikitoka shule mama anaweza kunipa pole?

Mwalimu: Sawa kabisa. Sasa tuangalie matumizi ya maneno haya matatu,

“niwie radhi”, “hongera”, na “asante”. Kumwia mtu radhi ni kumwomba mtu msamaha kwa sababu umemtendea vibaya. “Niwie radhi” inatumiwa sawa na “samahani”.

Juma: Mwalimu, sasa tafadhali nieleze juu ya matumizi ya “hongera”.

Mwalimu: Hongera hutumiwa kuonyesha jambo la furaha na sio la huzuni. Kwa mfano, wanafunzi wanapofaulu mitihani hupewa hongera na walimu wao na wazazi wao.

Mwalimu: Neno letu la mwisho ni “asante”. Hili hutumiwa wakati mtu mwingine anapokufanyia jambo zuri na pia unapopata huduma kutoka kwa mtu mwingine. Tena hutumiwa kumjibu mtu anapokuambia “pole,” “hongera”, au “tafadhali”.

Juma: Asante sana, mwalimu. Nimeelewa. Nitayatumia maneno hayo ya heshima kila siku.

Mwalimu: Sawa.

Juma: Kwa heri, mwalimu.

Mwalimu: Kwa heri.

Jibu maswali yafuatayo:

1. Je, neno “tafadhali” hutumiwa wakati gani?
2. Je, wakati gani tunatumia “samahani”, “niwie radhi” na “pole”?
3. Je, iko tofauti gani baina ya matumizi ya maneno haya matatu: “samahani”, “niwie radhi” na “pole”?
4. Eleza matumizi ya neno “hongera” na “asante”.
5. Tunga sentensi kwa kutumia maneno haya: “tafadhali”, “samahani”, “niwie radhi”, “pole” “hongera” na “asante”.
6. Jadili: umuhimu wa kutumia maneno ya heshima.

Heshima Kitu cha Bure

Heshima ni kitu chenye thamani kubwa mno katika maisha ya binadamu. Pamoja na thamani iliyonayo, heshima haigharimu chochote kwani haiuzwi wala hainunuliwi bali hutolewa bure na hali kadhalika hupokelewa bure yaani bila malipo/gharama. Vilevile siku zote malipo ya heshima huwa ni kuheshimiwa, ndio maana waswahili husema “jiheshimu utaheshimiwa”, na pia wahenga walisema “nipe nikupe”. Kwa hivyo, ukitaka kuheshimiwa ni lazima nawe ujiheshimu kwa kuwaheshimu watu. Heshima si kama maji ya mto, yaani yanaelekea upande mmoja tu. Heshima huelekea kote, juu na chini kwa wakubwa na wadogo.

Katika makabila mengi ya kiafrika kila jamii hufundishwa namna ya kuheshimiana, mdogo hutakiwa kumheshimu mkubwa na mkubwa huelekezwa namna ya kumheshimu mdogo.

Kwa mfano: mtoto akiamka asubuhi hutakiwa kumwamkia/kumjulika hali mkubwa akiwa ni baba yake, au mama yake, au kaka, dada na kadhalika. Na hali kadhalika wakati wa kula, mara nyingi mtoto hula na wazee wake ili apate kufundishwa heshima/adabu. Mtoto huwa hatakiwi kumtangulia mkubwa katika kunawa mikono, kula, na kuondoka kabla ya mkubwa wake. Na iwapo mtu mzima anarudi nyumbani kutoka kazini au safarini, mtoto hutakiwa kumkimbilia, kumsalimia na kumpokea iwapo ana mzigo. Ama mtu mzima huwa hatakiwi kusema maneno machafu mbele ya mdogo pia hatakiwi kumkaripia na kumpiga bila ya sababu za msingi.

Ama kweli heshima ni kitu chenye thamani, kwani jamii yenye kuheshimiana huwa na amani, utulivu na maelewano. Pia huepukana na ugomvi, chuki, uadui na utengano. Kwa vile heshima ni kitu cha bure basi

ni vizuri tuheshimiane.

Jibu maswali yafuatayo:

1. Kwa nini heshima ni kitu chenye thamani kubwa?
2. Eleza jinsi mtoto wa kitanzania anavyofundishwa namna ya kumheshimu mkubwa.
3. Eleza jinsi mtoto wa kichina anavyofundishwa namna ya kumheshimu mkubwa.

Msamiati

shoga (wa)	女友，女伴
Maka	麦加(伊斯兰教徒的朝圣地，在沙特阿拉伯西部)
-suka (kt)	编，织
-poa (kt)	恢复健康，病愈；冷却
-jikongoja (kt)	困难地行走；拄着拐杖走路
-afu (kt)	(用于祈求上帝)宽恕；治愈；保护；拯救，解救
salama salimini (kl)	平安无恙
-kirimu (kt)	款待；请客(吃饭)
ua (u)	(房屋后面用树、树枝或白铁皮围成的)院子
kutwa (n)	整天，全天
mwendo (mi)	速度；行程
-wia radhi (kt)	请求原谅，请求宽恕
hongera (n, kt)	祝贺，庆祝
kikumbo (vi)	撞击，推
-umiza (kt)	使人受伤

-udhi (kt)	烦扰；惹人生气
-kanyaga (kt)	踩，践踏（某物）
-kusudia (kt)	打算，决意
kusudi (ma)	目的，意图；有意，蓄意
-jali (kt)	顾及，注意；重视
-faa (kt)	合适；有用，有帮助
-gharimu (kt)	花费，开销
mhenga (wa)	古人；长老
-tangulia (kt)	走在前面；先行，领先
iwapo (kt)	如果，假如
-karipia (kt)	责骂，怒骂；申斥
utulivu (u)	宁‘静；安‘宁
maelewano (ma)	合意；和睦，相互理解
-epuka (kt)	避免，回避；躲开
ugomvi (u)	争吵；吵闹；不和
chuki (n)	憎恨，憎恶；厌恶
uadui (u)	敌意，敌视
utengano (u)	分离，分隔；分裂

Maelezo

1. wenyewe wapo? 此句意为主人在家吗？也可用 wenye nyumba wapo?
2. umeshindaje? 下午或晚上见面时的问候语。回答用 “salama” 或 “nimeshinda vizuri”。
3. kumjulia mtu hali 问候某人。等于 kumsalimia mtu。

4. Njema, zako tu? 省略了“habari”一词。此句的意思是: Habari zangu ni njema, sijui za kwako 或 kwangu ni salama nakuhofia wewe. (此种用法仅限于关系比较密切的人之间,并用于口语)。
5.hauchi unakucha 斯瓦希里语谚语: (原意)长夜总会天明。此处的意思是: 自然规律周而复始、永恒不变。引申义为: hali yangu haijabadilika 我的状况还是老样子。
6. Huonekani, kama uko Maka 等于 umeadimika sana。
7. Habari za kushinda au habari za kutwa? 与“umeshindaje”相同,用于一天结束时的问候语。可译为: 你今天过得怎么样?
8. Penye nia pana njia 斯瓦希里语谚语: 有志者必有路; 有志者事竟成。也可用: Penye nia ipo njia。
9. utaishi vizuri na watu 你将与人友好地相处。
10. “kupisha”是动词“kupita”的使役式。意为“使通过”,“让路”。
11. kumpiga mtu kikumbo 与人相撞,撞击某人。
12. kumkanyaga mtu bila kukusudia 不小心踩了某人,无意中踩了某人。也可用名词: kumkanyaga mtu bila ya makusudi。
13. wahenga walisema: “nipe nikupe”. 此处可译为: 古人云: “礼尚往来”。
14. Mtoto huwa hatakiwi kumtangulia mkubwa katika kunawa mikono. 坦桑尼亚人在用餐前通常要先洗手,洗手的顺序是先长辈后小辈,先宾客后主人。
15. “shikamoo”一词是小辈对长辈,下级对上级表示敬意的问候语,使用时不受时间的限制。回答用“marahaba”。
16. “chechei”一词是 12 岁以下的小孩对大人的问候语,回答仍用“chechei”。
17. subalkheri/sabalkheri! 早晨好! 回答仍用 subalkheri/sabalkheri!

例如：Subalkheri bibiye! Umeamkaje?

Subalkheri bwana mkubwa! Nimeamka salama.

Msalkheri/masalkheri! “下午好（晚上好）！回答仍用
“msalkheri/masalkheri”。

例如：Msalkheri babu! Habari za kushinda?

Msalkheri mjukuu wangu! Nimeshinda vyema, namshukuru

Mola. “subalkheri/sabalkheri”, “msalkheri/masalkheri” 等词
源于阿拉伯语，流行于桑给巴尔地区和东非沿海地区。

18. 坦桑尼亚人礼貌热情，见面时必须相互问候，小辈应该主动向长辈请安。坦桑尼亚有 120 多个民族，他们有着相同或各异的请安礼节。在一部分民族中，孩子给长者请安时，常常低头让长者抚摸其头部，表示请长者赐福于他。而在有的民族中则有着完全相反的风俗。孩子给长者请安时，长者俯身低头让孩子触摸其头顶，因为孩子像天使般的纯洁无邪，他们会给长者带来幸福。在一些地区，仍保留着妇女给长者和男人行屈膝礼的风俗，以示对他们的恭顺。

Methali za Kiswahili

Kutoa ni moyo, usambe ni utajiri.

送礼乃心意，切莫言富有。

Nifae la mvua, nikufae la jua.

你给我雨水，我给你阳光；礼尚往来。
